Mtu mwenye wajibu:	CEO	Toleo:	2.2
Imeidhinishwa na Bodi ya akurugenzi leo:	27 February 2019	Tarehe ya marekebisho yaliyopangwa:	Februari 2021

SERA G009: SERA YA KUFICHUA MAOVU

MAELEZO YA AWALI
Sera hii iliandikwa na So They Can (ya Kimataifa) nchini Australia kwa ajili ya matumizi ya taasisi zote za So They Can.
So They Can inaendesha taasisi tano zilizosajiliwa Australia, Kenya, Tanzania, New Zealand na USA, ambazo ni sehemu ya Muungano wa Kimataifa wa So They Can.
Katika Sera hii 'Mkurugenzi Mtendaji' ina maana ya Mkurugenzi Mtendaji wa So They Can (Kimataifa), So They Can Kenya na So They Can Tanzania. Isipokuwa kama itabainishwa vinginevyo 'Bodi' ina maana ya Bodi husika ya taasisi ya So They Can ambapo umeajiriwa au ulipo.

Ufafanuzi
1. **Ufichuaji wa maovu** unamaanisha kufichua kwa makusudi, hiari makosa ya mtu binafsi au shirika kunakofanywa na mtu ambaye ana taarifa za matukio mabaya au yale yanayotarajiwa kufanyika ndani ya shirika.

2. **Mfichuaji wa maovu** inamaanisha Mwakilishi yeyote ambaye anajaribu kufanya au anataka kutoa ripoti kuhusiana na kitendo kiovu chini ya sera hii na ambaye anataka kupatiwa ulinzi unaotolewa na sera hii.

3. **Tendo ovu** linajumuisha, lakini orodha hii inaweza kuongezeka:

- ukiukaji wa majukumu ya kisheria (ikiwa ni pamoja na uzembe, uvunjaji wa mkataba, uvunjaji wa sheria za utawala);
- Makosa ya jinai;
- Matumizi mabaya ya fedha;
- udanganyifu au tuhuma za udanganyifu;
- matumizi mabaya ya madaraka;
- ufichuaji unaohusu ukiukaji wa kutenda haki;
- kuhatarisha afya na usalama, ikiwa ni pamoja na hatari kwa umma na pia kwa wafanyakazi wengine;
- Uharibifu wa mazingira

Matumizi yasiyoidhinishwa ya fedha za shirika;

- Uwezekano wa udanganyifu na rushwa;
- unyanyasaji wa kingono na kimwili wa walengwa;
- matendo mengine yasiyo ya maadili; au
- kuficha jambo lolote kati ya yaliyoelezwa hapo juu.

4. **Wawakilishi wa So They Can** - ni watu wote na taasisi zote zinazofanya kazi kwa niaba ya So They Can bila kujali kama kuna au hakuna makubaliano rasmi ya kisheria kati yao na na So They Can. Hii inajumuisha, mbali na wenginge, wadhamini wote, wanachama, wakurugenzi, wafanyakazi, wakandarasi, washauri, wafanyakazi wa kujitolea, vibarua, wazabuni na washirika wanaotekeleza miradi bila kujali ni nchi gani majukumu yao yamepangwa.

SERA

Wakati wote So They Can itaendesha shughuli zake kwa weledi na uaminifu. Hata hivyo mashirika yote yanakumbana na hatari ya utendaji usio na weledi, tabia za jinai au menejimenti mbaya. So They Can inaamini kwamba ni wajibu wake kubaini hali hizo na kuchukua hatua kuzitatua.
So They Can imedhamiria kuweka mazingira ambayo wawakilishi watatiwa moyo kutoa taarifa za maovu na kwamba wanaweza kufanya hivyo katika mazingira salama.
Lengo la sera hii ni kuimarisha kanuni za msingi za So They Can kwa kuwajengea uwezo Wawakilishi wote kuripoti tendo lolote baya kwa nia nzuri.
Sera hii inalenga kutoa mfumo wa kuripoti na njia zinazoweza kutumika na Wawakilishi wote bila kujali mazingira yao ya kiofisi, wanaweza kuripoti mashaka ya maovu kutendeka.

Kanuni

1. Wawakilishi wote wa So They Can wanawajibu wa kufichua matendo mabaya au tuhuma za kutokea matendo mabaya kulingana na sera hii;

2. Wawakilishi wote wa So They Can wana haki ya kuongea kwa uhuru na ukweli ili kufichua vitendo viovu katika mazingira salama bila hofu ya kulipiziwa kisasi au kuadhibiwa; na

3. So They Can itashughulikia ufichuaji wa maovu kwa wakati, heshima na usiri.

4. So They Can itachukua hatua kuwalinda wafanyakazi wake dhidi ya kuonewa au kufukuzwa kazi kama wanaripoti kwa nia njema maovu au mashaka yanaashiria maovu yatatendeka.

Utekelezaji wa sera

1. Usiri

Ikiwa tendo baya au tuhuma za kutendeka kwa tendo baya zimeripotiwa chini ya sera hii, STC itahakikisha inalinda utambulisho wa mfichuaji wa tendo baya. Ili kutokuvuruga upelelezi wa tuhuma za kutendeka kwa tendo ovu, mfichuaji wa tendo hilo kutunza kwa siri taarifa walizozitoa, aina ya tendo ovu na utamvulisho wa watuhumiwa.
Kwa kawaida, STC haitatoa utambulisho wa mfichuaji isipokuwa:

- Mfichuaji anaridhia utambulisho wake uwekwe wazi;

- utambulisho unatakiwa na unaruhusiwa kisheria; na/au

- utambulisho ni wa muhimu kwa ajili ya uchunguzi zaidi .

Zaidi, taarifa zilizotolewa chini ya sera hii zitashughulikiwa kwa siri. Hata hivyo, wakati taarifa zinafanyiwa uchunguzi inaweza kuwa muhimu kubainisha maudhui yake kwa watu kama vile Mwakilishi mwingine, watu wa nje wanaofanya uchunguzi na, katika hali sahihi, vyombo vya sheria. Wakati fulani inaweza pia kuwa muhimu kufichua ukweli na kiini cha ripoti kwa mtu ambaye ripoti hiyo inamhusu. \
STC itachukua hatua za tahadhari kuhifadhi salama kumbukumbu yoyote inayohusiana na ripoti ya tendo ovu na watakaoweza kuzipata ripoti hizo ni wafanyakazi walioruhusiwa tu.
Kutoa taarifa inayohusiana na ripoti hiyo bila ruhusa, kama vile utambulisho wa mfichuaji itakuwa ni kosa kubwa ambalo linaweza kusababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu, ambazo ni pamoja na kufukuzwa kazi.

2. Ulinzi wa mfichuaji maovu
Hakuna mtu ambaye anafichua wasiwasi wa maovu kwa nia njema chini ya sera hii atakeyefukuzwa kazi au kupata madhara yoyote kutokana na kitendo hicho, hata kama mambo yaliyoibuliwa hayana msingi. Madhara ni pamoja kuadhibiwa isivyokubalika na kuonewa kwa njia zifuatazo pamoja na zinginezo:

- kufukuzwa;
- kushushwa cheo;
- aina yoyote ya unyanyasaji;
- ubaguzi;
- kutokutiliwa maanani sasa na badaye, au
- vitisho vya aina yoyote hapo juu.

Hatua yoyote ya kulipiza kisasi itachukuliwa kuwa ni utovu wa nidhamu mkubwa na itapelekea hatua za kinidhamu kuchukuliwa ambapo inaweza kuwa ni pamoja na kufukuzwa. Kama mfichuaji maovu anaamini hatua ya kulipiza kisasi dhidi yake imetendeka au ametishiwa, ana haki ya kuwasilisha suala husika kwa Bodi ya So They Can. Bodi ya So They Can inajitegemea (iko tofauti na timu ya usimamizi ya So They Can) na itatolea maamuzi suala hilo.

3. Wafichuaji maovu wanaohusishwa katika tendo ovu
Hata kama mfichuaji anahusishwa katika tendo ovu, hatatishiwa au kuonewa kwa kutoa ripoti chini ya sera hii.
Hata hivyo, kutoa ripoti haitakuwa kinga kwa mfichuaji uovu kukumbana na matokeo yanayotokana na ushiriki wake katika tendo baya. Katika baadhi ya mazingira kukiri inaweza kuwa ni sababu kupunguza makali ya adhabu au hatua nyingine.

4. Ufichuzi wa uongo
STC itauchukulia ufichuaji wa vitendo viovu kwa umakini mkubwa na kuwalinda wafanyakazi ambao wanaibua uovu kwa nia njema. Hata hivyo, wakati ulinzi hutolewa kwa wafichua maovu chini ya sera hii, taarifa za uongo zinazotolewa kwa makusudi hazitavumiliwa na mtu yeyote akipatikana anatoa madai au ripoti ya uongo atachukuliwa hatua za kinidhamu, ambazo ni pamoja kuachishwa kazi.

5. Utaratibu wa kutoa taarifa

So They Can inatumia jukwa lisilomtambulisha mpashaji habari la Whispli ambalo liko wazi kwa Wawakilishi wote kuripoti mashaka, maovu yanayoweza kutendeka au tabia mbaya za mtu au kikundi cha watu ndani ya shirika la So They Can kwa usalama kabisa.
Ili kuripoti tendo ovu, tabia mbaya au kuwasilisha malalamiko tafadhali nenda kwenye Fomu ya Matukio iliyoko kwenye jukwaa la Whispli kwa kutumia anwani https://app.whispli.com/SoTheyCan, vilevile inapatikana kwenye tovuti ya So They Can. Mfichuaji maovu anaweza kuchagua kutoa mawasiliano yake ambayo anayapata tu mchunguzi wa tukio, au kutotoa mawasiliano. Kwenye mfumo unaofanyakazi kupitia 256'bit encyption' utambulisho wa mfichua maovu kamwe hauwezi kuonekana. Vielelezo vya ziada kama picha, video na nyaraka zinaweza kuambatanishwa na Fomu ya Matukio.

Mara tu Fomu ya Matukio ikitumwa kupitia Whispli inatumwa na watumiaji wa Whispli ya So They Can (CFO na Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi na Hatari) kwa Mkurugenzi Mtendaji ambaye pia ni mtumiaji wa akaunti hii. Mkurugenzi Mtendaji anamjibu mlalamikaji kwa kumshukuru kwa kutoa mashaka yake na kuijulisha So They Can na kumjulisha kwamba suala hilo litachungunzwa.
Mkurugenzi Mtendaji atamwagiza meneja wa kesi kufanya uchunguzi. Bodi, Mkurugenzi Mtendaji au Mkurugenzi wa nchi husika atakuwa meneja wa kesi mwenye wajibu wa kufanya uchunguzi kwa mujibu wa:

- Kama malalamiko yanamhusu Mkurugenzi wa So They Can wa nchi Mkurugenzi Mtendaji ataendesha uchunguzi.
- Kama malalamiko yanamhusu Mkurugenzi Mtendaji, basi CFO na Mkuu wa ARC wataiagiza Bodi ya So They Can kufanya uchunguzi.
- Pale ambapo malalamiko hayamhusu Mkurugenzi Mtendaji, na lalamiko ni la hatari kwa kiasi cha kati au juu kwa kutumia jedwali la kipimo cha hatari lilicho kwenye Sera ya So They Can ya menejimenti ya hatari, Mkurugenzi Mtendaji ataijulisha Bodi ya Kimataifa ya So They Can na Bodi ya nchi husika juu ya lalamiko.

Meneja wa kesi atafanya tathmini ya awali kubaini kama taarifa ina mashiko na kuanza uchunguzi. Hii inawaweza kuhusisha kuwasiliana na mtoa taarifa kwa kutumia jukwaa la Whispli au njia nyingine kama maelezo yatatoa utambulisho. Meneja wa kesi ataijulisha Bodi ya So They Can na/au Mkurugenzi Mtendaji juu ya maendeleo ya uchunguzi.

Mara tu meneja wa kesi akimaliza uchunguzi wake na ripoti, menejiment na mtoa taarifa watajulishwa kilichojiri. Baada ya kukamilisha hili Meneja wa kesi atakabidhi kila kitu kwa Menejimenti ya juu ya So They Can kwa ajili ya hatua yoyote inayofuatia.
Pale ambapo lalamiko ni la hatari kwa kiasi cha kati au juu, CEO atamjulisha mlalamikaji na Bodi juu ya matokeo ya uchunguzi.

Wawakilishi wanaweza pia kuwasilisha mashaka yao kwa mdomo au kwa maandishi kwa meneja wake anayemsimamia, Mkuu wa mradi au Meneja wan chi, au, kama hajisikii huru kufanya hivyo, wana fursa ya kuwasilisha malalamiko yao moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mtendaji au Bodi ya Wakurugenzi, na wanatakiwa kutoa maelezo yanayojitosheleza pamoja na vielelezo stahiki ambavyo vinaweza kupatikana. Wanatakiwa wabainishe kwamba wanatumia Sera ya Kufichua maovu na kama wanataka utambulisho wao uwe siri. Watu wanaowasilisha malalamiko kwa maandishi wanatakiwa watumie fomu ya So They Can ya kuripotia matukio ambayo ipo kwenye Plani ya menejimenti ya matukio ya So They Can.

6. Namna ya kushughulikia taarifa za maovu

Siri zote zilizofichuliwa zitachukuliwa kwa umakini mkubwa na utaratibu ufuatao utatumika:

a) Mfichuaji wa siri ni lazima aweke wazi tangu awali, maslahi ya kibinafsi anayoweza kuwa nayo katika suala hilo. Hii ni pamoja na kutoa taarifa kamili ya kuhusika kwa mfichua siri katika jambo hilo.
b) Mtu ambaye taarifa zimepelekwa kwake atashughulikia ufichuzi (Meneja wa ufichuzi)
c) Meneja wa Ufichuzi atamtafuta mtu binafsi ambaye atapewa maelekezo ya kufanya uchunguzi kuhusu madai. Mtu anaweza kuwa wa ndani au nje ya So They Can. So They Can itaanza kufanya uchunguzi ndani ya wiki mbili tangu kutolewa kwa taarifa. Urefu na wigo wa uchunguzi utategemea suala lililofichuliwa. Katika matukio mengi, kutakuwa na tathmini ya awali ya taarifa ambayo itaamua kama kuna sababu ya uchunguzi wa kina kufanyika au kama taarifa, kwa mfano, taarifa zilizotolewa zimejikita katika maelezo ya uongo.
d) Mfichuaji wa maovu anaweza akatakiwa kutoa maelezo mengine wakati wa zoezi la uchunguzi.
e) Mchunguzi ataandaa ripoti ya uchunguzi ambayo itapitiwa na Meneja wa Ufichuzi.
f) Hatua sahihi itachukuliwa na Meneja wa Ufichuzi kwa kushauriana na mameneja waandamizi wahusika na timu ya watendaji. Hatua zinaweza kuwa ni pamoja na: kuanzisha mchakato wa hatua za kinidhamu, au kuwapa habari mamlaka ya nje kama kitendo cha uhalifu kimefanyika, kwa mfano, udanganyifu au wizi. Kama rufaa kwa mamlaka ya nje ni muhimu Bodi itashauriwa na Mfichuaji atapewa habari, ingawa ni kama So They Can inaona kuwa ni sahihi kufanya hivyo, rufaa hiyo inaweza kufanyika bila mfichuaji kujua au kuridhia.
g) Kama itabainika kuwa hakuna ushahidi wa kutosha wa kitendo viovu, au matendo ya mtu /watu siyo makubwa vya kutosha kuchukuliwa hatua za kinidhamu, inaweza kuwa sahihi kwa Meneja wa Ufichuaji kutumia njia isiyo rasmi kushughulikia jambo hilo. Katika hali hii matokeo yanaweza kuwa kwamba:

- madai hayajathibitishwa, au
- Hatua zinachukuliwa ili kuhakikisha kwamba tatizo halitokei tena.

(h) Kama mfichuaji maovu hakuridhika na majibu aliyopokea ana chaguo kuwasilisha jambo hilo moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mtendaji au mjumbe wa Bodi.

7. **Hatua za marekebisho na kufuata**
Kama madai yatakuwa hayajathibitishwa, kila juhudi zitafanywa kushughulikia madhara yoyote hasi juu ya sifa na ari ya mfanyakazi aliyehusika.

Kama sehemu ya uchunguzi wa ufichuzi uliofanywa chini ya sera hii, mapendekezo kwa ajili ya mabadiliko yatatolewa na mchunguzi ili kuiwezesha So They Can kupunguza hatari ya kurudia rudia kwa kitendo chochote kibaya kilichofichuliwa. Meneja wa Ufichuaji, au meneja mwandamizi atakayeteuliwa, atakuwa na wajibu wa kupitia na utekelezaji wa mapendekezo hayo.

8. **Menejimenti ya mtu ambaye ripoti ipo dhidi yake**
Kwa ujumla mtu ambaye ndiye mlengwa wa ripoti yoyote inayochunguzwa:

- Atapewa taarifa kuhusu tuhuma dhidi yake;
- Atapewa nafasi ya kujibu tuhuma kabla ya uchunguzi wowote kukamilika;
- Atafahamishwa kuhusu kiini cha maoni yoyote yasiyo mazuri kutoka kwa wachunguzi ambayo yanaweza kujumuishwa kwenye riopoti kabla ya uchunguzi kukamilika; na
- kuwa utetezi wao kuwekwa kwa haki katika ripoti yoyote.

STC inatambua kuwa wanaotuhumiwa pia lazima nao wapewe usaidizi wakati wa uchunguzi wa madai ya matendo maovu. So They Can itachukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba mtu ambaye ni mlengwa wa ripoti hiyo, anatendewa haki, hasa wakati wa mchakato wa tathmini na uchunguzi. Usaidizi unaotolewa na So They Can ni pamoja na kumpleleka kwa ajili ya ushauri nasaha.
Pale ambapo mtu ametajwa na mfichuaji maovu kama mtuhumiwa wa kitendo kiovu lakini upelelezi wa awali unabaini kwamba wasisasi wa mfichuaji hauna msingi na kwamba uchunguzi rasmi hauna haja kufanyika basi mfichuaji wa taarifa atajulishwa na jambo hili litafutwa.
Ambapo uchunguzi unashindwa kuthibitisha ripoti, matokeo ya uchunguzi na utambulisho wa mtu ambaye ni mlengwa wa ripoti lazima utunzwe kwa siri.

RELATED DOCUMENTS
So They Can Policy and Manual Register
So They Can Risk Management Policy
So they Can Incident management Plan – Incident Report